




Namna mbalimbali za kuunganisha punda na zana za kazi



Watatu bega kwa bega. Uunganisha punda waliolingana

Wawili mstari mmoja. Huu ni mfumo sahihi kwa kazi ya palizi.



Wanne bega kwa bega mistari miwili njia sahihi kwa kazi nzito za kulima na kuvuta mikokoteni mikubwa.



Kimechapishwa na:

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania (TARP II-SUA Project) (Uboreshaji matumizi endelevu ya wanyamakazi)

Chuo Kikuu Cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Chuo Kikuu, Morogoro.

Simu: 255-23-2600970
Au 255-23-2603511 ext.4251

Toleo Namba TS2-60



HATAMU ZA PUNDA



Hatamu ni nini?

Ni mikanda itumikayo kuongoza punda au farasi. Mikanda hii hutengenezwa kwa ngozi, turubai, kamba za katani na hata mipira. Ufungaji wa mikanda hutofautiana kulingana na aina ya kazi na pia idadi ya punda.

Hatamu ni muhimu sana katika uongozaji wa punda. Punda hufanya kazi kwa ufanisi zaidi pale afungwapo hatamu sahihi. Matumizi ya hatamu sahihi hupunguza maumivu kwa punda na kumuezesha kufanya kazi kwa muda mrefu zaidi.


Sehemu kuu za hatamu:

- * Shemire
- * Kiongoza kichwa
- * Kamba za hatamu
- * Mkanda wa kifua
- * Mkanda wa bega
- * Mkanda wa mgongoni
- * Mkanda wa nyuma



Hatamu bora ziwe na sifa zifutazo:

- * Gharama nafuu
- * Rahisi kutengenezwa
- * Imara na rahisi kutunza
- * Inayowiana na umbo la punda
- * Salama kwa mnyama na muongozaji

Shemire



Mkanda wa nyuma




Mkanda wa bega

Vipimo sahihi vya mikanda ya hatamu za punda (sentimeta):


Kifua	Urefu : 120	Upana : 7.5
Bega	60	5
Mgongo	60	5

Ufungaji sahihi wa hatamu Hatamu ya kichwani

Fuata kielelezo




Eneo sahihi kwa mkanda wa kifua




Kuunganisha punda mmoja na mkokoteni

Mikanda ya mgongoni na soji ni muhimu



Funga vyema mkanda wa kifua na ule wa breki/nyuma

Kuunganisha jozi ya punda na zana za kazi kwa kutumia swingo. Zingatia vipimo sahihi kama mchoro unavyoonesha. Swingo ni muhimu katika kuleta uwiano wa nguvu za kuvuta zana baina ya wanyama.



Hatamu na viunganishi sahihi huboresha ufanisi wa kazi, hupunguza majeraha kwa mnyama na pia huepusha ajali kwa watumiaji wa punda. Punda huonyesha ushirikiano zaidi pale anapovishwa hatamu sahihi.